



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA
CHUO CHA UALIMU BUTIMBA



Simu: +255768266944/+255784563045
Baruapepe: butimbatc@moe.go.tz
Tovuti: www.butimbatc.ac.tz

82 Barabara ya TTC,
S.L.P. 1411,
33116 MWANZA
Tarehe: 28 Mei, 2024

MAAGIZO KWA WANACHUO WA MWAKA WA PILI NA MWAKA WA TATU MUHULA WA KWANZA
UTAKAOANZA TAREHE 15 Julai, 2024

- Malipo ya ada** ni shilingi laki nne na nusu (450,000/-) tu kwa mwaka. Ada hii inaweza kulipwa kwa awamu mbili yaani **225,000/=** kwa muhula au ikalipwa kiasi chote **450,000/=** kwa mwaka. Ada ilipwe baada ya kupata namba ya kumbukumbu (Control number) kutoka kwa Mhasibu wa chuo ndugu **Makuru Mohamedi Temambele (0786441736)** au **Msajili (0755 646 138)/ (0689 363 690)**.
- Malipo ya **michango** mbalimbali yafanyike kwa mkupuo mmoja kwenye akaunti **Na. 31101200023** iliyopo **Benki ya NMB** yenye Jina **Butimba Teachers Training College**. Michango hiyo ni kama ifuatavyo:

NA	MCHANGO	KIASI	MAONI
i	Serikali ya wanachuo (SEWABU)	5,000	Kwa mwaka
ii	Huduma ya kwanza	10,000	Kwa mwaka
iii	Usafi na mazingira	20,000	Kwa mwaka
iv	Kukodisha godoro	10,000	Kwa mwaka
v	Michezo	30,000	Kwa mwaka
vi	Ulinzi	30,000	Kwa mwaka
vii	Ukarabati	25,000	Kwa mwaka
viii	Mtihani wa Utilifu (MOCK)	20,000	Ilipwe pindi unapofika chuoni
	JUMLA	150,000/-	

- Malipo ya ada ya Mitihani ya Taifa (NECTA) kwa wanachuo wa Mwaka wa pili miaka Miwili (2) na Mwaka wa Tatu miaka mitatu** kiasi cha shilingi **50,000/-** yafanyike kwenye akaunti ya benki ya **NMB** tajwa hapo juu kabla ya tarehe **28 Septemba, 2024**.
- Aidha, unaelekezwa kuzingatia mambo yafuatayo;**
 - Muhula mpya wa masomo unanza tarehe 15 Julai, 2024.
 - Mwanachuo afike chuoni na **Stakabadhi/Pay in Slip** mbili, moja ikionyesha malipo ya ada na nyingine ikionyesha malipo ya michango. Malipo ya ada na michango kamwe yasichanganywe. Mwanachuo atakayechanganya malipo hatarudishiwa fedha na atalazimika kufanya malipo upya.
 - Stakabadhi za malipo zioneshe jina kamili la mwanachuo analotumia chuoni na si jina la Mzazi au Mlezi** anayelipa.

- iv. Mwanachuo anaelekezwa kuripoti akiwa na Bunda (01) la karatasi (DOUBLE A/MONDI NO 1/MAPACHA).
- v. Iwapo mwanachuo anadaiwa ada, michango au kifaa chochote kwa mwaka wa masomo uliopita/iliyopita hakikisha unakamilisha kabla ya kurudi chuoni.
- vi. Mwanachuo hatapokelewa chuoni asipofika na maagizo tajwa hapo juu.
- vii. Mwanachuo anaelekezwa kuripoti chuoni kabla ya saa 12:00 jioni siku ya kufungua na si vinginevyo. **Hatua za kinidhamu zitachukuliwa kwa mwanachuo atakayechelewa.**

TANBIHI:

- A.** Wanachuo wote ambao hawajawasilisha vyeti halisi vya kuhitimu kidato cha Nne (Diploma Miaka 3) na kidato cha Nne na Sita (Diploma Miaka 2) hata kama hakikutumika kuomba kujiunga na mafunzo ya ualimu, wanaelekezwa kuwasilisha vyeti hivyo chuoni wakati wa kuripoti/kufungua chuo.
- B.** Kila mwanachuo anapaswa kuwa na kadi ya BIMA YA AFYA, Bima hii ishughulikiwe mwanachuo akiwa nyumbani na anaporipoti chuoni aonyeshe kadi ya Bima ya afya ofisi ya Usajili.



Nicholaus A Magige
MKUU WA CHUO

Nakala: Mwenyekiti wa Bodi ya Ushauri ya Chuo.